



TANGAZO KWA WATANZANIA DIASPORA DUNIANI - HADHI MAALUM.

TDC Global inawatangazia Watanzania diaspora duniani kuwa, Kamati Kuu ya TDC Global imeanza mchakato wa Hadhi Maalum kwa kuunda Kamati ya muda ya Hadhi Maalum.

Kamati ya mchakato wa hadhi maalum itakuwa na wajumbe ishirini (20), Kamati hiyo itakuwa na muda wa miezi miwili ya kukusanya maoni na mapendekezo ya watanzania diaspora duniani kupitia mikutano ya mitandao ya kijamii.

Kila mtanzania diaspora duniani na wale wote wenye nasaba za kitanzania, na familia zao wana haki sawa ya kutoa maoni yao. Tunapenda kuwajulisha Watanzania diaspora wote kwamba, wakati kamati husika ikitekeleza wajibu wake itaheshimu sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya nchi mwenyeji, ikiwemo GDPR

Miundo mbinu itakayotumika kukusanya maoni ni WhatsApp, Skype, Telegram, Zoom, barua pepe na njia nyingine zitakazoonekana zinafaa na kupendekezwa na Kamati ya Hadhi Maalum. TDC Global inawakaribisha diaspora wote kushiriki katika mchakato huu, na kusaidia kupatikana kwa Hadhi Maalum (Sera ya Diaspora ya Tanzania)

Wanachama watakaopenda kushiriki katika kamati hii wanaombwa wajiorodheshe kwa kutuma taarifa zao jina, namba ya simu, nchi ya makazi na maelezo mengine utakayoona yanafaa na uwe mwanachama hai wa TDC Global kabla ya terehe 25 June 2020 kwa barua pepe ya info@tdcglobal.org

Tunatanguliza Shukrani

TDC Global Pamoja Tunaweza.

Agnès P. Lerdorf
Mwenyekiti
Mahusiano ya Umma
2020-06-16

